

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



Simu: 026 2963533, Baruapepe: [info@moe.go.tz](mailto:info@moe.go.tz), Tovuti: [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz)

**NAFASI ZA MAFUNZO YA UALIMU  
NGAZI YA CHETI NA STASHAHADA KWA VYUO VYA SERIKALI NA VISIVYO VYA SERIKALI  
KWA MWAKA WA MASOMO 2017/2018**

**UTANGULIZI**

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatangaza nafasi za mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada kwa mwaka wa masomo 2017/2018. Masomo yataanza mwezi Septemba, 2017. Waombaji wa Mafunzo ya Ualimu Tarajali ambao watapenda kuajiriwa na Serikali wanapaswa wawe na umri usiozidi miaka 35 wakati wanapomaliza mafunzo yao. Aidha, waombaji wa mafunzo kazini ambao ni watumishi wa Serikali na wa mashirika binafsi hawatusiki na umri huu.

Kutokana na upungufu mkubwa wa walimu wa **Sayansi na Hisabati**, kipaumbele katika udahili kitatolewa kwa waombaji waliofaulu masomo hayo.

**Wahitimu wa Kidato cha Sita mwaka 2017 wanayo fursa ya kuomba kujiunga na mafunzo ya Stashahada ya Ualimu kwa mwaka 2017/2018.**

Kwa waombaji wa programu za Ualimu katika Vyuo vya Serikali watatakiwa kuomba kupitia tovuti ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ([www.nacte.go.tz](http://www.nacte.go.tz)) kwa kubofya kwenye "*Apply online (NOAVS)*" kisha kufuata maelekezo.

Kwa waombaji kwenye vyuo visivyo vya Serikali watatakiwa kuomba moja kwa moja kwenye vyuo husika. Vyuo visivyo vya Serikali vitadahili na kufanya uchaguzi wa wanafunzi wenyе sifa na kisha kuwasilisha NACTE majina ya waliochaguliwa kwa ajili ya uhakiki kabla ya kuyatangaza. Vyuo vinaelekezwa kuzingatia utaratibu wa udahili kwa mwaka wa masomo 2017/2018 uliotolewa na NACTE.

Maelekezo ya tangazo hili yanawahuwa waombaji wa mafunzo ya Ualimu katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali na Visivyo vya Serikali.

## A. MAFUNZO TARAJALI

Na.	AINA YA MAFUNZO	SIFA ZA KUJIUNGA	MUDA WA MAFUNZO
1.	Cheti Ualimu Elimu ya Msingi	<p>(a) Ufaulu wa Kidato cha 4 kwa kiwango cha daraja la I-III. Kipaumbele kitatolewa kwa waliofaulu masomo ya Hisabati, Fizikia au Sayansi ya Uhandisi (Engineering Science), Kemia, Baiolojia, Kiswahili na Kiingereza; na</p> <p>(b) Aliyehitimu Kidato cha 6 ni sifa ya nyongeza.</p>	Miaka 2
2.	Cheti Ualimu Elimu ya Awali	<p>(a) Ufaulu wa Kidato cha 4 kwa kiwango cha daraja la I-III Kipaumbele kitatolewa kwa waliofaulu masomo ya Hisabati, Kiswahili na Kiingereza; na</p> <p>(b) Aliyehitimu Kidato cha 6 ni sifa ya nyongeza.</p>	Miaka 2
3.	Cheti Ualimu Elimu kwa Michezo Msingi	<p>(a) Ufaulu wa Kidato cha 4 kwa kiwango cha daraja la I-III (Kipaumbele kitatolewa kwa waliofaulu masomo ya Hisabati, Baiolojia, Kiswahili na Kiingereza;</p> <p>(b) Mwenye uzoefu katika michezo ni sifa ya nyongeza (vithibitisho viambatishwe); na</p> <p>(c) Aliyehitimu Kidato cha 6 ni sifa ya nyongeza.</p>	Miaka 2
4.	Stashahada ya Ualimu Sayansi, Sayansi ya Jamii na Lugha	Ufaulu wa Kidato cha 6 kwa kiwango cha daraja la I-III na alama zisizopungua 'Principal Pass' mbili katika masomo yanayofundishwa katika shule za sekondari Kidato cha 1 hadi 4. Masomo yanayofundishwa katika shule za sekondari ni; Hisabati, Baiolojia, Kiswahili na Kiingereza, Historia, Jografia, Uraia, Kemia, Fizikia, Sayansi ya Kilimo, Biashara, Elimu kwa Michezo, Muziki, Uchoraji au 'Fine Art', Kiarabu, Kifaransa, Chakula na Lishe, na Sanaa za Maonesho.	Miaka 2
5.	Stashahada ya Ualimu Michezo, Muziki, Sanaa za Ufundii na Sanaa za Maonesho	<p>Ufaulu katika mtihani wa Kidato cha 6 kwa kiwango cha daraja la I-III na alama zisizopungua 'Principal Pass' mbili pamoja na ufaulu wa Kidato cha 4 katika masomo yafuatayo kwa kila kozi:</p> <p>(a) Sanaa za Ufundii: masomo ya Uchoraji pamoja na Kemia, Historia, Fizikia, Kiingereza, na Sayansi ya Uhandisi au 'Civil Engineering'.</p> <p>(b) Sanaa za Maonesho: masomo ya Sanaa za Maonesho pamoja Fasihi ya</p>	Miaka 2

		Kiingereza, Kiswahili, Jografia na Historia. (c) Muziki: masomo ya Muziki pamoja na Kiingereza, Kiswahili, Fizikia, Jografia na Historia; na (d) Elimu kwa Michezo: masomo ya Elimu kwa Michezo au ‘Physical Education’, Baiolojia, Kemia, Fizikia, Kiingereza’ na Kiswahili.	
6.	Stashahada ya Ualimu Ufundi	Ufaulu wa mtihani Kidato cha 6 kiwango cha daraja la I-III na alama zisizopungua ‘Principal Pass’ mbili katika masomo ya Baiolojia, Kemia, Fizikia, Hisabati na Jografia.	Miaka 2
		Mhitimu aliyesomea Cheti cha Ufundi (NTA ngazi ya 6)	Mwaka 1
7.	Stashahada ya Ualimu Kilimo	Ufaulu wa mtihani Kidato cha 6 kiwango cha daraja la I-III na alama zisizopungua ‘Principal Pass’ mbili katika masomo ya Sayansi ya Kilimo na Baiolojia au Kemia.	Miaka 2
		Mhitimu mwenye ufaulu wa Stashahada ya Kilimo na Mifugo	Mwaka 1
8.	Stashahada ya Ualimu Biashara	Ufaulu wa mtihani wa Kidato cha 6 kwa kiwango cha daraja la I-III na alama zisizopungua ‘Principal Pass’ mbili katika masomo ya Biashara ‘Accounts’ and ‘Commerce’.	Miaka 2
9.	Stashahada ya Ufundi Sanifu wa Maabara	Ufaulu wa mtihani Kidato cha 6 kwa kiwango cha daraja la I-III na alama zisizopungua ‘Principal Pass’ mbili katika masomo mawili kati ya yafuatayo: Fizikia, Baiolojia, Sayansi ya Kilimo na Kemia.	Miaka 2

## B. MAFUNZO KAZINI

1.	Cheti Elimu Maalum	(a) Mwalimu kazini aliyeptitia mafunzo ya ualimu Daraja A; (b) Uzoefu wa kazi ya ualimu usiopungua miaka 2; na (c) Aliyefaulu angalau somo moja la Sayansi katika mtihani wa Kidato cha Nne.	Mwaka 1
2.	Stashahada ya Ualimu Elimu Maalum	(a)Mwalimu mwenye Stashahada ya Ualimu fani ya Sayansi au Sayansi ya Jamii na uzoefu kazini usiopungua miaka miwili; na (b)Mwalimu anayefundisha watoto wenyewe mahitaji maalumu (wasioona, viziwi, wenyewe ulemavu wa akili nk) ni sifa ya nyongeza (vithibitisho viambatishwe).	Miaka 2
3.	Stashahada ya Ualimu Michezo, Muziki, Sanaa	Ufaulu wa mtihani Kidato cha 6 kwa kiwango cha daraja la I-III na alama zisizopungua ‘Principal Pass’ mbili kwa kuzingatia masomo yafuatayo kwa	Miaka 2

<p>za Ufundi na Sanaa za Maonesho</p>	<p>kila kozi:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>a) Sanaa za Ufundi: masomo ya 'Fine Art' pamoja na ufaulu wa Kidato cha Nne masomo ya Baiolojia, Historia, Fizikia, Kiingereza na Ufundi Ujenzi au 'Civil Engineering';</li> <li>b) Sanaa za Maonesho: masomo ya Sanaa za Maonesho pamoja na ufaulu wa Kidato cha 4 masomo ya Fasihi ya Kiingereza, Kiswahili, Jografia na Historia.</li> <li>c) Muziki: masomo ya Muziki pamoja na ufaulu wa Kidato cha Nne masomo ya Kiingereza, Muziki, Fizikia, Jografia, Historia na Kiswahili;</li> <li>d) Elimu kwa Michezo: masomo ya Elimu kwa Michezo pamoja na ufaulu wa Kidato cha Nne kwenye masomo ya Baiolojia, Kemia, Fizikia, Kiingereza na Kiswahili.</li> </ul>	
---------------------------------------	---	--

**Tanbihi: Masomo ya Dini** hayatatumika kama kigezo cha sifa ya kijiungu na Mafunzo ya Ualimu.

### **MAELEZO MUHIMU/ VIAMBATISHO**

- (i) Waombaji wa Mafunzo ya Ualimu kwa **Vyuo vya Ualimu vya Serikali** watume maombi yao kwa njia ya kielektroniki NACTE kupitia tovuti [www.nacte.go.tz](http://www.nacte.go.tz);
- (ii) Waombaji wa mafunzo katika **Vyuo vya Ualimu vya Serikali** watachagua vyuo hadi vitano (5) ambavyo wangependelea kwa kuanza na kila mwombaji anachokipenda zaidi;
- (iii) Walimu Kazini watapaswa kuonesha barua ya ruhusiwa kwenda kusoma kutoka kwa waajiri wao watakapo kuwa wanaripoti chuoni;
- (iv) Majibu kwa watakaochaguliwa kijiungu na Mafunzo ya Ualimu yatatolewa kupitia tovuti ya NACTE ([www.nacte.go.tz](http://www.nacte.go.tz)), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ([www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz)) na katika katika vyuo vya Ualimu; na
- (v) Barua za kijiungu na Mafunzo zitatolewa na chuo atakapongwa mwombaji kwa kutumia anuani yake.

**MWISHO WA KUWASILISHA MAOMBI NI TAREHE 14/08/2017**

**LIMETOLEWA NA  
OFISI YA KAMISHNA WA ELIMU  
KITENGO CHA MAFUNZO YA UALIMU  
PROGRAMU ZA MAFUNZO YA UALIMU 2017/2018**